TANGAZO LA SERIKALI NA. 586 la tarehe 30/9/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu vya 6(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE ZA MWAKA, 2022

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke za mwaka, 2022.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa na mtu kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri kwa mujibu wa sheria ndogo hizi;

"Afisa Masuuli" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote atakaye idhinishwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Afisa Mwidhiniwa" Maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;"

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Temeke;

"Bango" maana yake ni kitu chochote chenye matangazo au ujumbe maalumu kitakacho chimbiwa ardhini;

"Eneo la Burudani" maana yake ni mahali popote ndani ya eneo la Halmashauri ambapo shughuli ya burudani inafanyika;

"Kibali' inamaanisha idhini au ruhusa inayotolewa kwa maandishi na mamlaka ya Halmashauri;

"Leseni" maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa mtu binafsi, Kampuni au Taasisi, kinachoruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote halali katika eneo la Halmashauri.

"Machinjio" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama au ukaguzi wa nyama na ukaushaji wa ngozi kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.

"Masoko" maana yake ni maeneo maalumu yaliyotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaa au huduma kufuatana na taratibu zilizowekwa na Halmashauri;

"Mifugo" maana yake ni wanyama wote wanaofugwa na binadamu itajumuisha ngombe, mbuzi, kndo, nguruwe, punda, kuku, bata na wanyama wengine wafugwao;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi;

"Mkataba" maana yake ni makubaliano yenye

nguvu ya kisheria ya ununuzi au uuzaji au utoaji wa huduma yoyote kati ya Halmashauri na wadau wa Halmashauri;

"Mnada" maana yake ni sehemu au eneo lilipata kibali cha Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa;

"Stendi au Egesho" maana yake ni ene lolote la kuegesha magari katika eneo la mamlaka ya Halmshauri;

"Ushuru wa Madini ya Ujenzi" maana yake ni Ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumaru, Kifusi, Udongo Mfinyanzi au chochote kinachochimbwa katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, Kampuni au Shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Halmashauri;

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika biashara, huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoorodheshwa kwenye **Jedwali la kwanza** Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla yaliyopo katika kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo, Halmashauri itatoza Ada na Ushuru katika vyanzo vifuatavyo:-

(i) Ushuru wa kukodisha mali za Halmashauri;
(ii) Ada ya usajili wa uchimbaji wa madini na usafirishaji wa madini kwa uzito;
(iii)Ada ya kupima Afya;

(iv) Ada ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi;

(v) Ada na Vibali mbalimbali;

(vi) Vibali vya mazao yanayotokana na Misitu;

(vii) Ada ya kuendesha shughuli za Utamaduni, Burudani na Michezo;

(viii) Ushuru wa kushusha na kupakia mizigo katika masoko na maeneo mengine ya Halmashauri

(ix) Ada ya stendi, egesho, kulaza na kuosha magari.

(x) Ada ya ukaguzi wa nyama na ngozi.

(xi) Ada ya usajili wa vikundi vya kijamii.

(xii) Ushuru wa viingilio.

(xiii) Ada ya kibali cha kusimika bango.

(xiv) Ada ya mashauri katika mabaraza ya kata

Namna ya kukusanya Ada na Ushuru

5. (1) Halmashauri itaweka utaratibu itakavyoona inafaa ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalum ya kutoza Ada na Ushuru kutoka vyanzo vya mapato kama ilivyoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi.

(2) Malipo ya Ada au Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliofanyika.

(3) Ada na Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni au kibali husika.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 5 cha Sheria Ndogo hizi Halmashauri au Wakala kwa idhini ya Afisa

Masuuli itatoa kwa mlipaji stakabadhi halali ya kawaida kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(5) Afisa Mwidhiniwa ana uwezo wa kuingia katika jengo lolote la mmiliki au mtumiaji wakati wowote kwa lengo la kukusanya Ada au Ushuru.

(6) Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo ameshindwa kulipa Ada au Ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(7) Endapo bidhaa au mali iliyokamatwa na Halmashauri au Wakala haitalipiwa Ushuru unaodaiwa ndani ya siku 7 kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka, na ndani ya siku 2 kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka. Halmashauri itakuwa na uwezo baada ya kupata idhini ya Mahakama kuuza bidhaa au mali na fedha zitakazopatikana Halmashauri itakata pesa inayodaiwa na kiasi kinachobakia atarudishiwa mmiliki.

(8) Afisa Mwidhiniwa ana uwezo wa kumkamata bila hati ya kukamata na kumshtaki mtu yeyote anayetakiwa kulipa ada endapo atakuwa hajalipa Ada au Ushuru.

(8) Kwa namna yoyote ile Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri.

Wajibu wa kulipa Ada au Ushuru

6. (1) Ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru kulipa kiwango cha Ada au Ushuru kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au

mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(3) Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu atakayelipa Ada au Ushuru kutunza kumbukumbu za malipo.

Kibali au leseni

7. (1) Halmashauri itatoa kibali au leseni kwa mfanyabiashara au mtu yeyote kwa kadri itakavyoona inafaa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu kwa kila mfanyabiashara au mtu yeyote anayetaka kufanya jambo lolote linalohitaji kibali au leseni kuomba na kupata leseni au kibali kutoka Halmashauri.

Uteuzi wa Wakala

8. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kwa maandishi Mtu binafsi, Kampuni au Taasisi iliyosajiliwa kuwa Wakala wake kwa ajili ya kukusanya Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa wakala

9. Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

(a) Kukusanya na kupokea Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alililopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) Wakala atakusanya Ada au Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa

10. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:-

(1) Atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada au Ushuru.

(3) Atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada au Ushuru ndani ya Halmashauri.

(5) Atashindwa kutoa taarifa sahihi au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ada au Ushuru.

(6) Atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

Adhabu

11. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (200,000.00) na isiyozidi Shilingi Milioni Moja (1,000,000.00) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Uwezo wa Mkurugenzi kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari yake mwenyewe kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye **Jedwali la Pili** la Sheria Ndogo hizi na kulipa Ushuru anaodaiwa pamoja na faini ya kiasi cha shilingi Laki Mbili (200,000.00).

GN Na. 261 ya 2018

13. Sheria Ndogo za (Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, GN Na. 261 ya 15/06/2018 zimefutwa.

GN Na. 64 ya 2018

14. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Stendi) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, GN Na. 64 ya 15/06/2018 zimefutwa.

GN Na. 263 ya 15/06/2018

15. Sheria Ndogo za (Ada ya Upimaji na Ukaguzi wa ramani za Viwanja) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, GN Na. 263 ya 15/06/2018 zimefutwa.

GN Na. 262 ya 2018

16. Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko na Magulio) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, GN Na. 262 ya 15/06/2018 zimefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 4 (1))

A: USHURU WA KUKODISHA MALI ZA HALMASHAURI

NA.	AINA YA CHANZO	KIASI CHA USHURU/ADA	MUDA
1.	Catapillar, Motor Grader na Wheel loader	i. Tsh.800,000/= kwa taasisi za kibiashara ,serikali na kampuni	Saa nane
		ii. Tsh. 400,000/= kwa wananchi wakazi wa eneo husika.	Saa nane
2.	Gari la Halmashauri	Tsh. 500,000/=	Kwa siku
3.	(i)Nyumba za Halmashauri za kupangisha kwa ajili ya makazi	Asilimia 14 ya thamani ya nyumba ya kuishi.	Kwa mwaka
	(ii) Nyumba za Halmashauri za kupangisha kwa ajili ya biashara	Asilimia 18 ya thamani ya nyumba ya biashara .	Kwa Mwaka
4	Ukumbi wa Halmashauri	500,000/=	Kwa siku
5	Kumbi zilizopo katika shule za Halmashauri	300,000/=	Kwa siku
6.	Uwanja wa Halmashauri	500,000/=	Kwa siku
7	Vizimba, frem na vibanda vya biashara	Viwango kulingana na bei ya soko ya eneo husika ya kupangisha vizimba,	Kwa mwezi

		frem au kibanda ambavyo vita pitishwa na Halmashauri.	
8	Kumbi zilizopo kwenye ofisi za kata	200,000/=	Kwa siku
9	Mali zingine zinazomilikiwa na Halmashauri	Kiwango kitatokana na masharti ya mkataba husika.	

B: ADA YA USAJILI WA UCHIMBAJI WA MADINI NA USAFIRISHAJI WA MADINI KWA UZITO

NA.	CHANZO	KIASI TSH.	MUDA/KIPIMO
i	Usajili wa umiliki wa madini ya mchanga na kifusi	300,000/=	Mwaka
ii	Usajili wa Umiliki wa madini ya kokoto,moramu na chokaa	300,000/=	Mwaka
iii	Usafirishaji madini kwa uzito chini ya tani 7	3000/=	Kwa tripu
iv	Usafirishaji madini kwa uzito wa tani 8-10	5000/=	Kwa tripu
v	Usafirishaji madini kwa uzito zaidi ya tani 10	10,000/=	Kwa tripu

C: ADA YA KUPIMA AFYA

NA.	AINA YA CHANZO	KIASI	MUDA
1.	Ada ya kupima wahudumu kila mhudumu wa nyumba ya kulala wageni, hoteli, mgahawa,saluni,wafanyakazi wa viwanda vya kuzalisha vinywaji, wauzaji wa vyakula, vilivyopikwa au kukaangwa anawajibika kusajili kwa Halmashauri ili kubainisha ukamilifu wa afya yake kuendesha shughuli husika	10,000/=	Kila baada ya miezi 6
2	Wafanyakazi wa viwanda na biashara nyingine zisizokuwa za vyakula	10,000/=	Kwa mwaka

D: ADA YA MABADILIKO YA MATUMIZI YA ARDHI

NA.	AINA YA VIWANJA	KIASI Tshs.
A	MAKAZI KUWA BIASHARA	
	1. Makazi ya Famili zaidi ya moja	
	i. Makazi ya Familia 2 hadi 4	100,000
	ii. Makazi ya Familia 5 hadi 6	200,000
	iii. Makazi ya Familia 7 hadi8	200,000
	iv. Zaidi ya 10	300,000
	2. Makazi na Biashara ya maduka	200,000
	3. Ofisi	50,000

Tangazo La Serikali Na.. 586 (Linaendelea)

	4. Huduma	450,000
	5. Karakana (service trade)	450,000
	6. Viwanda	450,000
	7. Makazi Biashara na Ofisi	250,000
	BIASHARA	
	1. Makazi ya Familia zaidi ya moja	
	i. Mgahawa	250,000
	ii. Nyumba ya kulala wageni	300,000
	iii. Hotel	700,000
	iv. Maduka makubwa(super market	1,000,000
	v. Kituo cha mafuta	450,000
	vi. Kumbi	500,000
	vii. Baa	
B	KARAKANA (SERVICE TRADE)	
	1. Makazi ya Familia Zaidi ya moja	
	i. Makazi ya Familia 2 hadi 4	200,000
	ii. Makazi ya Familia 5 hadi 6	300,000
	iii. Makazi ya Familia 7 hadi 8	300,000
	iv. Zaidi ya 10	400,000
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	300,000
	3. Ofisi	200,000
	4. Huduma	100,000
	5. karakana (service trade)	500,000
	6. viwanda	1,000,000
	7. Makazi Biashara na Ofisi	300,000
	8. BIASHARA	
	a) Ngahawa	200,000
	b) Nyumba ya kulala wageni	300,000
	c) Hotel	700,000
	d) Maduka makubwa (Super market	700,000
	e) Kituo cha mafuta	1,000,000
	f) Kumbi	500,000
	f) Baa	500,000
C	HUDUMA	
	1. Makazi ya Familia zaidi ya moja	
	a) Makazi ya familia 2 hadi 4	500,000
	b) Makazi ya familia 5 hai 6	700,000
	c) Makazi ya familia 7 hadi 8	800,000
	d) Makazi ya familia 9 hadi 10	1,000,000
	e) Zaidi ya 10	1,200,000
	2. Makazi za Biashara ya maduka	700,000
	3. Ofisi	1,000,000
	4. Huduma	200,000
	5. Karakana (Service trade)	1,500,000
	6. Viwanda	2,000,000
	7. Makazi Biashara na Ofisi	700,000
	8. BIASHARA	
	a) Mgahawa	800,000
	b) Nyumba ya kulala wageni	850,000

Tangazo La Serikali Na.. 586 (Linaendelea)

	c) Hoteli	1,000,000
	d) Maduka makubwa (Super market)	1,000,000
	e) Kituo cha mafuta	1,200,000
	f) Kumbi	1,000,000
	g) Baa	1,500,000
D	MAKAZI PEKEE	
	1. Makazi Familia zaidi ya moja	
	a) Makazi ya familia 2 hadi 4	200,000
	b) Makazi Familia 5 hdi 10	300,000
	c) Zaidi ya 10	500,000
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	300,000
	3. Ofisi	400,000
	4. Huduma	100,000
	5. Karakana (service trade)	500,000
	6. Viwanda	1,000,000
	7. Makazi Biashara na Ofisi	400,000
	8. BIASHARA	
	a) Mgahawa	300,000
	b) Nyumba ya kulala wageni	400,000
	c) Hoteli	1,000,000
	d) Maduka makubwa (super makert)	1,000,000
	e) Kituo cha mafuta	1,200,000
	f) Kumbi	1,000,000
	g) Baa	1,500,000
E	OFISI	
	1. Makazi ya familia zaidi ya moja	
	a) Makazi ya Familia 2 hadi 4	200,000
	b) Makazi ya Familia 5 hadi 10	300,000
	c) Zaid ya 10	500,000
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	300,000
	3. Ofisi	400,000
	4. Huduma	100,000
	5. Karakana (Service trade)	500,000
	6. Viwanda	500,000
	7. Makazi Biashara na Ofisi	600,000
	8. BIASHARA	
	a) Mgahawa	300,000
	b) Nyumba ya kulala wageni	300,000
	c) Hoteli	1,000,000
	d) Maduka makubwa(supermakert)	1,000,000
	e) Kituo cha mafuta	1,000,000
	f) Kumbi	1,200,000
	g) Bar	1,000,000
F	VIWANDA	
	1. Makazi ya Familia zaidi ya moja	
	a) Makazi ya Familia 2 hadi 4	200,000
	b) Makazi ya Familia 5 hadi 10	300,000
	c) Zaidi ya 10	500,000
	2. Makazi na Biashara ya Maduka	300,000
	3. Ofisi	400,000

Tangazo La Serikali Na.. 586 (Linaendelea)

	4. Huduma	100,000
	5. Karakana (Service trade)	500,000
	6. Viwanda	1,000,000
	7. Makazi Biashara na Ofisi	500,000
	BIASHARA	
	a) Mgahawa	300,000
	b) Nyumba ya kulala wageni	300,000
	c) Hoteli	1,000,000
	d) Maduka makubwa (supermarket)	1,000,000
	e) Kituo cha mafuta	1,200,000
	f) Kumbi	1,000,000
	g) Baa	1,000,000
G	NYONGEZA YA SAKAFU	
	Ada italipwa kwa kuzingatia eneo la mraba (Square metre) la sakafu ya jengo iliyoongezeka	60,000 hadi 1,200,000

E: ADA NA VIBALI MBALIMBALI

NA	AINA YA CHANZO	KIASI TSH.	MUDA
1	Ada ya fomu za maombi ya zabuni (Kitaifa)	100,000/=	Kwa ombi
2	Ada ya fomu za maombo ya zabuni (Kimataifa)	300,000/=	Kwa ombi
3	Kibali cha kuweka kontena la biashara futi 40	500,000	Kwa mwaka
4	Kibali cha kuweka kontena la biashara futi 20	250,000	Kwa mwaka
5	Kibali cha kuweka kioski	200,000/=	Kwa ombi
6	Kibali cha Upimaji	100,000/=	Kila kiwanja
7	Huduma ya Kupima Ardhi kwa kila kiwanja kilichopimwa kwa Makampuni Binafsi	100,000/=	Kila kiwanja
8	Ada ya Maombi ya kiwanja	50,000/=	Kila ombi
9	Nukuu ya bei (Quotation)	50,000/=	kila fomu
10	Kibali cha uzio:-		Kwa ombi
	a. Eneo dogo(High Density)	100,000/=	
	b. Eneo la Kati(Medium Density)	150,000/=	
	c. Eneo Kubwa(Medium Density)	300,000/=	
11	Kibali cha kuzungusha mabati (hoarding).	5000/= hadi 10000/=	Kwa urefu futi moja
12	Kibali cha kubomoa:-		Kwa ombi
	a. Eneo dogo(High Density)	100,000/=	
	b. Eneo la Kati(Medium Density)	150,000/=	
	c. Eneo Kubwa(Medium Density)	300,000/=	
	d. Mnara wa simu	150,000/=	
13	Kibali cha ujenzi wa mnara wa simu.	300,000/=	
14	Ada ya ukaguzi wa Ramani		
	a. Kiwanja kikubwa(law density)	50,000	
	b.Kiwanja cha kati (medium density)	30,000	
	c. Kiwanja kidogo (high density)	10,000	

	d. Viwanda na hoteli	500,000	
15	Kibali cha ujenzi	Asilimia 0.3 ya thamani ya kiwanja.	
16	Fomu ya maombi ya kiwanja	10,000/=	
17	Kupata barua ya toleo ya kiwanja	20,000/=	
18	Kuonyeshwa kiwanja	50,000/=	
19	Huduma ya ukaguzi wa uchimbaji msingi	50,000/=	
20	Huduma ya ukaguzi wa jengo	50,000/=	
21	Huduma ya ukaguzi wa ukuta hadi wall plate	50,000/=	
22	Huduma ya ukaguzi wa upauaji na upigaji bati	50,000/=	
23	Maombi ya hati ya kuingia kwenye jengo	50,000/=	

F: ADA YA VIBALI VYA MAZAO YANAYOTOKANA NA MISITU

NA	AINA YA CHANZO	KIASI TSH.	MUDA
1	Duka la mbao	51,000/=	Kwa mwaka
2	Duka la mkaa		
3	Duka la Kuni		
4	Kiwanda cha samani(funiture)		
5	Nguzo		
6	Magogo		
7	Vinyago		
8	Duka la Miti		
9	Yadi ya Mbao		
10	Fito		
11	Gunia la mkaa (mfuko wa kg 28)	500/=	Kila gunia
12	Gunia la mkaa (mfuko wa kg 56)	1,000/=	
13	Viwanda vya mbao (woodworks factory) vyenye ukubwa wa kuchakata mbao chini ya 5,000m3 kwa mwaka	102,000/=	Kwa mwaka
14	Viwanda vya mbao (woodworks factory) vyenye ukubwa wa kuchakata mbao zaidi ya 5,000m3 kwa mwaka	200,000/=	Kwa mwaka
15	Kukata miti ya hifadhi kupisha ujenzi(maendelezo)	50,000/=	Kila ombi
16	Lori la Mkaa	2,000/=	Kila lori
17	Lori la Mbao	3,000/=	

G: KIBALI CHA KUKATA/KUVUNA MITI ASILI KATIKA MAENEO YA WANANCHI KWA MADHUMUNI YA BIASHARA

NA	DARAJA	USHURU KWA MITA ZA UJAZO (M3) KWA MITI ILIYOSIMAMA TSH.
1	Daraja A	52,000/=
2	Daraja B I	47,000/=
3	Daraja B II	35,000/=
4	Miti ya madaraja yote kwa matumizi ya kuni	2,000/=

H: KIBALI CHA KUKATA/KUVUNA MITI YA KUPANDWA KATIKA MAENEO YA WANANCHI KWA:

1	Matumizi ya Biashara	5,000/=
2	Kuni	2,000/=

I: ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO

Na	Aina ya Chanzo	Kiasi Tsh.	Muda
1	Tamasha lenye hadhi ya Kitaifa	200,000/=	Kwa siku
2	Tamasha lenye hadhi ya Kimkoa	100,000/=	
3	Tamasha lenye hadhi ya Kiwilaya	50,000/=	
4	Tamasha lenye hadhi ya Kata	30,000/=	
5	Tamasha lenye hadhi ya Mtaa	20,000/=	
6	Waombaji wa kibali cha burudani ndani ya ukumbi	5% ya gharama za ukumbi	
7	Waombaji wa kibali cha burudani nje ya Ukumbi	50,000	
8	Kibali cha kusherehesha (MC)	100,000/=	Kwa mwaka
9	Kibali cha kutoa huduma ya chakula na mapaambo kwenye burudani	100,000/=	Kwa mwaka
10	Matangazo kwa kutumia vyombo (promosheni)	50,000/=	Kwa siku
11	Kibali cha banda au ukumbi wa video	100,000/=	Kwa mwaka
12	Pool table na Play station	50,000/=	Kwa mwaka

J: USHURU WA KUSHUSHA NA KUPAKIA MIZIGO KATIKA MASOKO NA MAENEO MENGINE YA HALMASHAURI

NA.	AINA YA CHANZO	KIASI TSHS.	UKUBWA UJAZO
1	Dagaa	1000/-	Kwa kila gunia/kiroba lisilo na lumbesa/kishungi
2	vitunguu	1000/-	
3	Viazi mbatata	1000-	
4	Viazi vitamu	1000-	
5	magimbi	1000-	

Tangazo La Serikali Na.. 586 (Linaendelea)

6	Maembe mviringo	1,000/-	700/ roba/gunia
7	Maembe dodo	1,000	150/ roba/gunia
8	Mabungo	1,000	Tenga/box
9	Nyanya	1,000/-	box
10	Pilipili	1000/	Kwa kila gunia/kiroba lisilo na lumbesa/kishungi
11	Karoti	500/	
12	Matango	1000/	
13	Ndimu	500/	
14	Limao	500	
15	Passion	1000	
16	parachichi	1000	
17	Peasi	500	
18	Ndizi mbivu	500	Box/tenga
	Ndizi mkungu	500	
19	Machungwa	500	200/ tenga
20	Mihogo	1,000	
21	Papai	500	tenga
22	Nazi kubwa	1000	300/ gunia
23	Nazi ndogo	1000	350/ gunia
24	Samaki wakavu	1000	
25	Samaki wabichi	1000	
26	Matikiti	1000	15/tenga
27	Nanasi kubwa	1000	20/Tenga
28	Nanasi ndogo	1000	25/tenga
29	Kabichi	1000	25/tenga
30	Stafeli	1000	50/tenga
31	Nyanya chungu	1000	Kwa kila gunia/kiroba lisilo na Lumbesa/ kishungi
32	Kunde	1000	
33	Njegere	1000	
34	Mkaa	1000	
35	Karanga	1000	
36	Maharage		
37	Tangawizi		
38	Ulezi		
39	Mahindi		
40	Kuku	1,000	Tenga
41	Miwa	10,000	Lori
42	Na bidhaa au zao lolote ambalo halijatajwa	1000	Gunia/kiroba
	LORI LENYE BIDHAA ZA VIWANDANI	**TSHS.**	**KWA GARI**
43	Tani 1 hadi 2	30,000	
44	Tani 3 hadi 7	50,000	
45	Tani 8 hadi 12	100,000	
46	Tani 13 na Zaidi	150,000	
47	Lori la Mbao/Mirunda Tani 1 hadi 2	30,000	
48	Lori la Mbao/Mirunda Tani 3 hadi 7	50,000	
49	Lori la Mbao/Mirunda Tani 8 hadi 12	100,000	
50	Lori la Mbao/Mirunda Tani 13 na zaidi	150,000	

K: GARI INAYOINGIZA MIZIGO AU KUPAKIZA MIZIGO SOKONI NA MAENEO MENGINE YA HALMASHAURI

NA.	AINA YA USHURU	KIWANGO CHA USHURU TSHS
	A- VYOMBO VYA USAFIRI	
1	Guta	1,000
2	Toyota/susuki/carry – 500kg	4,000
3	Gari tani 1 pick up	6,000
4	Gagri tani 1.5	7,500
5	Gari tani 2	12,000
6	Gari tani 3	14,000
7	Gari tani 4	16,000
8	Gari tani 7	20,000
9	Gari tani 8-10	25,000
10	Gari tani 15	30,000
11	Gari au contena zaidi ya tani 10	35,000
	B - USHURU WA KUTWA KATIKA MASOKO	
12	Vizimba	500
13	Bucha	1000
14	Duka	1000
15	Baba/mama lishe	500
16	Mitumba	500
17	Kuku hai	1000
18	Maeneo mengine	500

L: USHURU WA STENDI, EGESHO, KULAZA NA KUOSHA MAGARI

(a) Ushuru wa stendi

NA.	AINA YA GARI	KIWANGO TSHS
1	Gari dogo	1,000
2	Daladala	2,000
3	Mabasi makubwa ya mikoani	5,000
4	Teksi (cab taxes)	1,000
5	Magari makubwa ya mizigo	3,000
6	Bodaboda (pikipiki ya kubeba abilia)	1,000
7	Bajaji (kwa ajili ya kubeba mizigo na abilia)	1,000

(b) Ushuru wa kuegesha magari katika maeneo ya Halmashauri

NA.	AINA YA GARI	KIWANGO TSH.	MUDA
1	Gari dogo	500/=	kwa saa na haitazidi Tshs. 2,000/- kwa siku
2	Daladala		
3	Mabasi makubwa ya mikoani		
4	Teksi (cab taxes)		
5	Magari makubwa ya mizigo		

6	Bodaboda (pikipiki ya kubeba abilia)		
7	Bajaji (kwa ajili ya kubeba mizigo na abilia)		

(c) **Ada ya kibali cha kuosha na kulaza magari kwa mtoa huduma**

NA.	AINA YA ADA	KIASI TSHS.	MUDA KWA MWAKA
1	Kuosha magari	50,000	
2	Kulaza magari	100,000	

M: USHURU WA UKAGUZI WA NYAMA NA NGOZI

NA.	AINA YA MIFUGO	USHURU WA UKAGUZI WA MNYAMA KABLA YA KUCHINJWA TSH.	USHURU WA UKAGUZI WA MNYAMA BAADA YA KUCHINJWATSH.	USHURU WA KAGUZI WA NGOZI TSH.
1	Ngamia	3000/=	5000/=	1,000/=
2	Ng'ombe	2,500/=	2,500/=	1,000/=
3	Mbuzi/kondoo	1,000/=	1000/=	500/=
4	Punda	2,000/=		500/=
5	Nguruwe	1500/=	1500/=	-
6	Wanyama wadogo (sungura, simbilisi)	500/=	500/=	-
7	Wanyama aina ya ndege (kuku, bata)	250/=	250/=	-

N: ADA YA USAJILI WA VIKUNDI VYA KIJAMII

NA	AINA YA ADA/USHURU	KIWANGO	MUDA
1	Ada ya kikundi cha kijamii	20,000	Kwa mwaka

O: USHURU WA VIINGILIO

NA.	AINA YA ADA/USHURU	KIWANGO TSH.	MUDA WA KULIPA
1	Maonyesho, michezo au mikutano au tukio lolote ambalo washiriki wake watatozwa viingilio.	Asilimia 5% ya makusanyo ya viingilio	Ndani ya siku 30 kuanzia siku ya tukio
2	Iwapo mtu yeyote au kampuni au taasisi binafsi italipa gharama za viingilio	Asilimia 5% ya kiwango cha viingilio vilivyolipwa.	Ndani ya siku 30 kuanzia siku ya tukio

P: ADA YA KIBALI CHA KUSIMIKA BANGO

NA.	AINA ZA ADA	KIWANGO TSH.	MUDA
1.	Fomu ya Maombi	10,000/=	Kwa ombi

2.	Kwa kila mita moja ya mraba	10,000/=	Kwa mwaka

JEDWALI LA PILI

KUFIFILISHA KOSA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 12)

Mimi……. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwamba mnamo tarehe……ya mwezi……..mwaka …….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ……cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke za mwaka 2022.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…ya mwezi……Mwaka…….

Jina……..…..

Saini……..….

Mbele ya:

Jina……..

Cheo……

Saini……..……..

Tarehe: …….

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitiwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kilichofanyika tarehe 21 mwezi wa 03 mwaka 2022

ELIHURUMA SAMWEL MABELWA
Mkurugenzi
Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

ABDALLAH SAID MTINIKA
Mstahiki Meya
Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

NAKUBALI

L.S

Dodoma
19 Septemba, 2022

INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB)
Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa